

Swahili Transcript:

Nicholaus:Kuna hatua zozote ambazo, kuna mtu anayefanya hatua zozote za kuweza kufanya suluhisho la hilo tatizo kwamba watu wamesikia sana, kwamba jinsi gani unaendelea kwamba jinsi gani watu waendeleo, kwamba ile walivyobadilishwa mwenendo wabaki vilevile sio kwamba baada ya muda ni kitu ambacho umeshazoea kukisikia kwamba halafu unarudia ulivyokuwa mwanzo?

Mtoa mada:Kuna mambo mbalimbali wanajaribu kufanya, kwa mfano, kuna vitu kama kuwatumia watu ambao, vijana ambao wameathirika na virusi vya ukimwi. Ile ni moja ya changamoto, kuna vijana mbalimbali sasa hivi wanapata support mbalimbali ili waweze kuwaeleza vijana wao wakiwa kama waathirika wa virusi vya ukimwi, kwamba uhalisia ukoje, hili ni jambo la kwanza ambalo wanalifanya na linasaidia, kwa sababu ukikutana na kijana mwenzako wa miaka hiyohiyo halafu ana virusi vya ukimwi halafu anakueleza, na kitu cha namna ile, matarajio yake na vitu vya namna ile, inasaidia kidogo kuwachemsha vijana kwamba kumbe virusi vya ukimwi hata vijana ambao wako katika umri wa namna ile wanao, unaona? Kwa hiyo, hicho ni kitu kimojawapo kinafanyika. Kitu kingine ni kuna vitu kama kujaribu kuonyesha vitu kama, wanatumia hizi nini..role plays, michezo ya kuigiza na vitu vya namna hiyo, wanajaribu kuifanya zaidi kuonyesha uhalisia wa maisha ya vijana, namna wanavyopata virusi vya ukimwi, kuna mashirika mbalimbali ambayo wanajaribu kusema pengine hiyo itawavutia vijana, kwamba kijana anaona maisha halisi ya kijana yalivyo na namna halisi ambavyo huyu kijana anapata virusi vya ukimwi, na namna halisi ambavyo maisha yake yanakuwa. Kwa hiyo wanajaribu kuleta ile picha ili iweze kukukumbusha zaidi kwamba kwa sababu ukiona kitu ambacho unaona kabisa, una-imagine kwamba pengine ninaweza nikawa mimi kwamba maisha ya kawaida, kwamba huyu mtu anapata virusi vya ukimwi katika hali ya kawaida, hiyo na yenyewe ni moja ya njia wanajaribu kuleta, wataalamu wanajaribu kuisogeza kwa jamii ili kusudi, kwa vijana zaidi ili kusudi waweze kufanyaje? Kushtuka kwamba eehe tuko kwenye hatari, hiki ni kitu kingine. Na bado ni kuendelea kwa sababu sio kwamba wanafanya kitu kimoja wanaacha, bado ile taarifa bado inaendelea kutolewa. Kwa hiyo bado elimu ya ukimwi bado wanaendelea kuitoa siku hadi siku ili kuweza kufanyaje? kuweza kuhakikisha kwamba haya mambo yote yanakwenda pamoja. Lakini bado kuna mambo mengine ambayo nadhani yanaweza yakafanyika ambayo yanaweza yakasaidia pengine. Na moja ya vitu ambavyo sasa hivi serikali imeanza kulitilia mkazo kwa mfano kama serikali ni kwamba wanasema nini.. hizi stadi za maisha zinaanza kupewa mkazo zaidi kwenye mitaala ya kishule, ili kwa wale vijana ambao tayari wako kwenye mashule waweze kujua ni namna gani ya kujikimu na kujikinga na virusi vya ukimwi. Kwa hiyo hicho ni kitu kingine ambacho wanakipigia debe, kwa mfano sasa hivi kuna kitu serikali inakisema kwamba peer education au elimu rika inatakiwa iwe ni moja ya kitu cha lazima kwenye kila shule. Na katika hilo, masuala ya elimu rika inasaidia zaidi kwa sababu taarifa nyingi vijana wanazipata kupitia vijana wenzao. Kwa hiyo ukiweza kuwafundisha kikundi kidogo cha vijana, ukaweza kuwapa

taarifa nzuri na ukaweza kuwajenga wakawa kama sijui kwa Kiswahili tunasemaje, lakini role models hawa; wakawa watu wa kuigwa kwenye kundi kubwa la vijana, ile inasaidia na yenyewe kwa sababu wale wanaweza wakafikisha ujumbe kwa haraka kwa wenzao kuliko ikitumika kama mwalimu na mwanafunzi, kwa hiyo hicho ni kitu kingine ambacho wanajaribu kuhakikisha kwamba kinasukuma mabadiliko katika vijana. Kwa hiyo hilo ni jambo lingine ambalo ninaweza kusema kwamba lipo sasa hivi linafanyiwa kazi

English translation:

Nicholaus: Are there any programs that help people stay faithful so they do not get the HIV/AIDS virus? People have already heard about HIV/AIDS and how people get AIDS. So what do you do to make sure that they do not engage in activities which will put them at risk of getting the virus?

Presenter: There are many things they try to do, like introducing young people to those who are already infected with AIDS. That is a big challenge for young people, because they see the reality of HIV/AIDS from their peers who are infected with HIV/AIDS. When young people see their friends being infected, that makes them aware of AIDS. They see other people who are their age with AIDS. They realize it is possible even for them to get AIDS, when they see how people get AIDS in normal circumstances. So that is the first thing they confront.

The second thing people do is to use role play to portray real life situations of how people get AIDS. There are some organizations that believe role play will inspire many young people and prevent them from getting AIDS. When people meet young people with HIV/AIDS infections and understand how they got infected and how their lives have changed simply by being infected, that is a lesson on how to prevent themselves from getting HIV. So learning by seeing is another method used by experts to relay the message of HIV/AIDS to the public and to make them aware of the virus.

That is an ongoing activity. They do not do this one time and stop for a while. No, they continue giving this AIDS education everyday. But there is still more to be done to help people be more aware of HIV/AIDS. One of the things the government is doing now is to insist that health education be taught in our school curriculums. Students can learn how to provide for themselves and sustain their needs so they can prevent themselves from getting AIDS. Some people got AIDS out of economic desperation. In order to get money for their needs, they engaged in prostitution, and as a result, they got infected.

Another program the government has initiated is that peer education should be implemented in every school. Peer education is good because most young people get information about AIDS from their peers. If you teach a small group about AIDS, and they get the clear message about AIDS, they themselves become good models for their fellow students. They will help spread the message more easily than by using teachers to spread the word. This is what is going on to make sure young people get enough

information about AIDS, and not only that, but that they also change their way of life and keep from being infected.

About CultureTalk: CultureTalk is produced by the Five College Center for the Study of World Languages and housed on the LangMedia Website. The project provides students of language and culture with samples of people talking about their lives in the languages they use everyday. The participants in CultureTalk interviews and discussions are of many different ages and walks of life. They are free to express themselves as they wish. The ideas and opinions presented here are those of the participants. Inclusion in CultureTalk does not represent endorsement of these ideas or opinions by the Five College Center for the Study of World Languages, Five Colleges, Incorporated, or any of its member institutions: Amherst College, Hampshire College, Mount Holyoke College, Smith College and the University of Massachusetts at Amherst.

© 2003-2008 Five College Center for the Study of World Languages and Five Colleges, Incorporated